## FUNZO LA 18

1. Mungu alimwambia Nuhu kuwa alipanga kuleta gharika ili kuwaangamiza watu wote wasiomwamini Mungu.
-Je, Mungu husahau kufanya kile alipanga kufanya?
-La.

2. Je, Mungu hufanya kile alisema atafanya?
-Ndiyo.

3. Je, Mungu alisubiri kwa muda gani ili watu wa wakati wa Nuhu wamwamini?
-Miaka 120.

4. Je, Mungu alipokuwa akiwasubiri watu wamwamini, hasira zake kwa dhambi zao zilipunguka?
-La.
-Mungu alipokuwa akiwasubiri watu wamwamini, hasira yake kwa dhambi zao iliongezeka.

5. Mungu alimwambia Nuhu afanye nini alipomaliza kujenga safina?
-Mungu alimwambia Nuhu achukue jamii yake na waingie katika safina.
-Mungu alimwambia Nuhu pia achukue wanyama ndani ya safina.

6. Je, Nuhu na jamii yake waliingia vipi kwenye safina?
-Kupitia kwa mlango wa pekee.



7. Je, wanyama wote waliingia vipi katika safina?
-Kupitia kwa mlango wa pekee.

8. Baada ya Nuhu, jamii yake na wanyama kuingia katika safina, je, ni nini kilichofanyika?
-Mungu alifunga mlango.

9. Kwa nini Mungu alifunga mlango?
-Ili walio ndani wawe salama.
-Ili walio nje wafe.

10. Je, yeyote aweza kuepuka adhabu ya Mungu?
-La.

11. Je, Mungu aliwezaje kufanya mafuriko yafunika ardhi yote?
-Ili kufanya mafuriko yafunike ardhi yote, Ili kufanya mafuriko yafunike ardhi yote, Mungu aliyafanya maji yote yaliyokuwa katika anga kunyesha chini.

12. Je, watu walikuwa wameona mvua awali?
-La.

13. Je, nini kiliwafanyikia wanyama wote nje ya safina?
-Walikufa wote.

14. Je, nini kiliwafanyikia watu wote waliokuwa nje ya safina?
-Walikufa wote.

15. Je, kuna yeyote katika safina aliyekufa?

-La.

16. Je, ni ishara ipi ambayo Mungu alimpa Nuhu na watu wote?
-Upinde wa mvua.

17. Je, ishara ya upinde wa mvua inamaanisha nini?
-Upinde wa mvua unamaanisha kuwa Mungu hataiharibu dunia tena na mafuriko.

18. Je, Mungu ametimiza ahadi yake ya kutoiharibu dunia kwa mafuriko?
-Ndiyo.

19. Je, wana wa Nuhu ambao ni baba wa watu wote ulimwenguni ni nani?
-Shemu, Hamu, and Yafethi.

-Baada ya Mungu kumuokoa Nuhu kutokana na mafuriko, miaka mingi sana ilipita.

-Miaka mingi ilipita, watoto wengi wakazaliwa, hadi watu wengi wakaishi katika ardhi.

-Je, watu waliozaliwa baada ya Nuhu ni nani?

-Hao walikuwa mababu wako na mababu wangu.

-Je, mababu wetu walijua kuhusu Mungu?
-Ndiyo.



-Je, mababu wetu walijuaje kuhusu Mungu?

-Kwanza, mababu wetu walijua kuhusu Mungu kwa sababu wazee waliwaambia watoto habari za Mungu na mafuriko.

-Je, wazee waliwaambia nini watoto kuhusu Mungu na mafuriko?

-Wazee waliwaambia watoto kuwa Mungu anachukia dhambi, na hivyo basi, aliwaharibu watu wote isipokuwa Nuhu na jamii yake.

-Je, mababu wetu walijuaje tena kuhusu Mungu?

-Pili, mababu wetu walijua kuhusu Mungu kupitia upinde wa mvua.

-Je, upinde wa mvua uliwaambia nini mababu wetu kuhusu Mungu?

-Ya kuwa Mungu anawapenda watu, na kuwa hatawaangamiza watu tena kwa gharika.

-Je, mababu wetu walijuaje tena kuhusu Mungu?

-Tatu, mababu wetu walijua kuhusu Mungu kwa sababu anga, milima, mito, na miti iliwaambia kuhusu Mungu.

-Je, anga, milima, mito, na miti iliwaambia nini mababu wetu kuhusu Mungu?

-Ya kuwa Mungu pekee ni Mungu, na kwambu watu wamfuate Mungu pekee.

-Je, upinde wa mvua unatuambia kuhusu Mungu leo?
-Ndiyo.

-Je, anga, milima, mito, na miti hutuambia leo kuhusu Mungu?
-Ndiyo.

-Ijapokuwa mababu wetu walijua kuhusu Mungu, je, wengi wao walimwamini Mungu?
-La.

-Ni wachache kati ya mababu wetu waliomwamini Mungu.

-Badala ya kumfuata Mungu, wengi wa mababu wetu walimfuata nani?

-Wengi wa mababu wetu walimfuata Shetani na uongo wake.

-Wengi wa mababu wetu walitawaliwa na Shetani.

-Je, Shetani aliwaambia mababu wetu wafanye nini?

-Shetani aliwaambia mababu wetu watolee jua, mwezi na nyota dhabihu.

-Shetani pia aliwaambia mababu wetu watolee dhabihu roho za miti, roho za mito, na roho za wafu.



-Mababu wetu walichonga sanamu za mbao na mawe zinazofanana na watu na wanyama na wakazitolea dhabihu.

-Shetani alikuwa akiwaongoza mababu wetu wasimwamini Mungu.

-Shetani alikuwa akiwaongoza mababu wetu kumuasi Mungu.

-Shetani alikuwa akiwaongoza mababu wetu kutolea dhabihu jua, mwezi na nyota.

-Shetani alikuwa akiwaongoza mababu wetu kutolea dhabihu roho za miti, mito, na za wafu.

-Shetani hataki yeyote amuabudu Mungu.

-Mababu wetu hawakutaka Mungu awaongoze.

-Mababu wetu walitaka kumfuata Shetani na watu wengine pekee.

-Baada ya mafuriko, mmoja wa mababu wetu ambao watu walimfuata ni Nimrodi.

-Nimrodi aliwaamuru watu kujenga miji mingi.

-Mojawapo ya miji aliyowaamuru kujenga ulikuwa unaitwa Babeli.

-Katika mji wa Babeli, Nimrodi aliwaamuru watu kujenga

mnara mrefu ambao ungemfikia Mungu.

Tusome Mwanzo 11:1-4

1-Nchi yote ilikuwa na lugha moja na usemi mmoja.
2-Ikawa watu waliposafiri pande za mashariki waliona nchi tambarare katika nchi ya Shinari; wakakaa huko.
3-Wakaambiana, Haya, na tufanye matofali tukayachome moto. Walikuwa na matofali badala ya mawe, na lami badala ya chokaa.
4-Wakasema, Haya, na tujijengee mji, na mnara, na kilele chake kifike mbinguni, tujifanyie jina; ili tusipate kutawanyika usoni pa nchi yote.

-Mungu aliwaambia Adamu na Hawa waijaze dunia, na waishi katika sehemu tofauti katika dunia.

-Mungu pia alimwambia Nuhu aijaze dunia, na kuishi sehemu tofauti katika dunia.

-Je, ni kwa nini Mungu hakutaka watu wote waishi katika sehemu moja duniani?

-Mungu hakutaka watu wote waishi katika sehemu moja ili wasimsahau Mungu.

-Mungu hakutaka watu wote waishi katika sehemu moja ili dhambi zao zisiwe nyingi sana.



-Mungu alitaka watu waijaze dunia, lakini watu walitaka kuishi pamoja katika sehemu moja.

-Watu hawakutaka kuishi sehemu tofauti duniani.
-Watu walitaka kuishi pamoja.

-Kwa hivyo, watu wote wakahamia kwa mji wa Babeli, na wakaanza kujenga mnara mrefu.

-Je, ni kwa nini watu waliaza kujenga mnara mrefu Babeli?

-Kwa sababu watu walikuwa na kiburi sana.
-Kwa sababu watu walitaka kujifanyia jina wenyewe.

-Je, watu walipoanza kujenga mnara, Mungu aliona?
-Ndiyo.

Tusome Mwanzo 11:5

5-Bwana akashuka ili auone mji na mnara waliokuwa wakiujenga wanadamu.

-Mungu aliona kuwa watu walikuwa wakijenga mnara.
-Mungu anaona kila kitu.

-Mungu anaona watu wote kila mahali.
-Mungu anaona kila mmoja wenu kila wakati.

-Je, Mungu anayajua mawazo ya watu?
-Ndiyo.

-Kabla hata mtu kuanza kuwaza, Mungu anayajua mawazo ya huyo mtu hadi mwisho.

-Je, Mungu anayajua maneno yote ya watu wote?
-Ndiyo.

-Kabla hata mtu kuanza kusema neno, Mungu anayajua maneno yake hadi mwisho.

-Je, Mungu anayajua matendo yote ya watu wote?
-Ndiyo.

-Kabla ya mtu kuanza kutenda jambo, Mungu anajua atakachofanya hadi mwisho.

-Watu walidhani kuwa Mungu aliwasahau.

-Je, Mungu huwasahau watu?

-Mungu hasahau mawazo ya watu.
-Mungu hasahau wanachosema watu.
-Mungu hasahau wanachofanya watu.

-Je, Mungu alisema nini alipoona kuwa watu hawamtii?

Tusome Mwanzo 11:6-7

6-Bwana akasema, Tazama, watu hawa ni taifa moja, na lugha yao ni moja; na haya ndiyo wanayoanza kuyafanya, wala sasa hawatazuiliwa neno wanalokusudia kulifanya.



7-Haya, na tushuke huko, tuwachafulie usemi wao ili wasisikilizane maneno wao kwa wao.

-Kwa sababu mababu wetu hawakumtii Mungu, Mungu aliamua kuwaadhibu.

-Je, ni adhabu gani ambayo Mungu aliwapa?
-Mungu aliwapa lugha tofauti ili wasielewane.

-Je, ikiwa Mungu angewapa watu lugha tofauti, wangeweza kuelewana?
-La.

-Je, ikiwa Mungu angewapa watu lugha tofauti, wangemaliza kujenga mnara?
-La.

-Je, ikiwa Mungu angewapa watu lugha tofauti, wangeweza kuishi sehemu moja?
-La.

-Zamani za kale, mababu wetu waliongea lugha moja.

-Lakini kwa sababu mababu wetu walikataa kumtii Mungu na kujaza dunia, Mungu akawapa lugha tofauti.

-Hapo Babeli, Mungu aliwapa watu wote lugha tofauti.

-Lugha ya Kiingereza ilianzia Babeli.

-Lugha ya Kifaransa ilianzia Babeli.
-Lugha ya Kiispania ilianzia Babeli.

-Lugha zote ilianzia Babeli.

-Baada ya Mungu kuwapa watu wote lugha tofauti, je, Mungu alifanya nini tena?

Tusome Mwanzo 11:8-9

8-Basi Bwana akawatawanya kutoka huko waende usoni pa nchi yote; wakaacha kuujenga ule mji.
9-Kwa sababu hiyo jina lake likaitwa Babeli; maana hapo ndipo Bwana alipoichafua lugha ya dunia yote; na kutoka huko Bwana akawatawanya waende usoni pa nchi yote.

-Baada ya Mungu kuwapa watu wote lugha tofauti, Mungu aliwatawanya watu wote katika sehemu tofauti duniani.

-Mungu alitaka watu waijaze dunia, lakini watu walitaka kuishi sehemu moja.

-Je, watu walishinda au ni Mungu alishinda?
-Mungu alishinda.

-Je, yeyote aweza kupigana na Mungu na ashinde?
-La.

-Je, Mungu atawafanyia nini wote ambao watapigana dhidi yake?



-Atawaadhibu.

-Mungu aliwatawanya watu katika sehemu tofauti duniani.

-Baadhi yao walihamia karibu.
-Baadhi yao walihamia mbali zaidi.

-Je, mababu wako walifika vipi huku?

-Baada ya miaka mingi sana, mababu wako walikuja hapa kwa miguu na kwa mashua.

-Hivi ndivyo watu wenu waliaza.

-Hivi ndivyo watu wengi duniani waliaza.

-Mababu wako walikuwa Babeli.

-Mababu wangu walikuwa Babeli.

-Mababu wa kila mtu walikuwa Babeli.